# CHUO CHA USTAWI WA JAMII

DAR ES SALAAM & KILIMANJARO




# JARIDA LA MTANDAONI

## APRILI - JUNI, 2025



Katibu Mkuu WMJJWMM Dkt. John Jingu akitoa pongezi kwa wanafunzi wa ISW waliojiunga na programu za ubunifu, Dar es salaam 17 Aprili, 2025.

# DKT. JOHN JINGU: VIJANA TUMIENI PROGRAMU ZA UBUNIFU NA UANAGENZI KUJIAJIRI NA KUSAIDIA JAMII

**Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (WMJJWMM), Dkt. John Jingu amesema programu za ubunifu, uanagenzi na ushauri nasihi ni fursa muhimu za ajira kwa vijana nchini. Amewahimiza vijana kuzitumia ili waweze kujiajiri na kuajiri wengine baada ya kuhitimu masomo yao.**

**Akizungumza alipokuwa ziarani Chuo cha Ustawi wa Jamii tarehe 17, Aprili 2025, Dkt. Jingu aliwataka wanafunzi kushiriki kikamilifu kwenye programu zinazotatua changamoto za kijamii ili elimu yao ilete matokeo chanya kwa jamii.**

**Alisisitiza kuwa wanafunzi ni "mainjinia wa mabadiliko" na programu hizi ni nafasi adhimu kwa ajira, hivyo wasizichukulie kimzaha. Pia aliwahimiza kusoma kwa bidii darasani na kutumia teknolojia kuboresha huduma kwa jamii na kushirikiana na wadau mbalimbali.**



Katibu Mkuu WMJJWMM Dkt John Jingu (mwenye suti ya bluu) akikagua ujenzi wa ukumbi wa mihadhara ISW, Dar es salaam 17 Aprili 2025.

**Dkt. Jingu alipongeza Chuo kwa ubunifu wa kuanzisha mitaala mipya inayokidhi mahitaji ya soko la ajira. Pia alikagua ujenzi wa ukumbi wa mihadhara na kuhimiza ubora na ukamilishaji kwa wakati.**

**Kwa upande wake, Mkuu wa Chuo Dkt. Joyce Nyoni alisema Chuo kimeandaa mitaala mipya minne na kuongeza programu mpya 15 zitakazoanza kutumika katika mwaka wa masomo 2025/2026.**




Picha ya Watumishi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii kabla ya kuelekea katika maandamano Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi yaliyofanyika Tanganyika Packers, Dar es salaam 01 Mei, 2025.

# WATUMISHI WA ISW WASHEREKEA MEI MOSI

**Watumishi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii, Kampasi ya Dar es Salaam, walijumuika kwa shangwe na furaha kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi tarehe 1 Mei, 2025. Maadhimisho hayo yalifanyika katika viwanja vya Tanganyika Packers, Kawe, Dar es Salaam na kuhudhuriwa kwa wingi na watumishi kutoka Kampasi ya Dar es salaam. Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mhe. Albert Chalamila.**




Picha ya Watumishi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii katika maandamano ya Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi yaliyofanyika Tanganyika Packers, Dar es salaam 01 Mei, 2025.



Wakufunzi wa ISW wakipata mafunzo ya mfumo mpya wa Digital Books Library yaliyofanyika Chuo cha Ustawi wa Jamii, Dar es salaam 09 Mei, 2025.

# WANAFUNZI ISW KUSOMA VITABU WAKIWA POPOTE KWA MFUMO WA BUKU

**Katika jitihada za kuimarisha upatikanaji wa maarifa kwa njia ya kidijitali, Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW), kupitia Kampasi yake ya Dar es Salaam, kiliendesha mafunzo kwa wakufunzi kuhusu matumizi ya mfumo mpya wa Digital Books Library unaosimamiwa na BUKU Platform, tarehe 9 Mei 2025. Mafunzo hayo yalifunguliwa rasmi na Naibu Mkuu wa Chuo (Taaluma), Prof. Sotco Komba.**

**Mfumo huu wa kisasa unalenga kuwawezesha wanafunzi zaidi ya 5,000 wa ISW kupata vitabu kwa njia ya mtandao bila ya kizuizi cha muda au mahali walipo. Kupitia BUKU Platform, wanafunzi na wakufunzi wataweza kufikia rasilimali mbalimbali za kielimu kwa urahisi zaidi, hatua inayotarajiwa kuongeza ubora wa ufundishaji na ufanisi katika taaluma.**

**Kupitia matumizi ya teknolojia hii ya kisasa, Chuo kinaendelea kuunga mkono mageuzi katika elimu ya juu kwa kupunguza utegemezi wa vitabu vya karatasi pekee na kupanua wigo wa upatikanaji wa elimu jumuishi, hususan kwa wanafunzi waliopo katika kampasi ya Kisangara na maeneo mengine ya mbali. Mfumo huu pia ni chachu ya kuimarisha utamaduni wa kujisomea na kufanya tafiti kwa kutumia vyanzo sahihi na vinavyoaminika.**



isw_official_tz isw_official_tz taasisiyaustawi isw_official_73 www.isw.ac.tz



Prof. John Philemon akiwa anatoa mafunzo yanayohusu Uandishi wa Kitaaluma kwa wakufunzi yaliyofanyika Chuo cha Ustawi wa Jamii, Dar es salaam.

# ISW YAWEKEZA KATIKA UBORA WA TAFITI KUPITIA MAFUNZO YA UANDISHI WA KITAALUMA

**Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW), kupitia Kampasi yake ya Dar es Salaam, kilitoa mafunzo maalum ya Uandishi wa Kitaaluma (Capacity Building on Academic Writing) kwa wakufunzi. Mafunzo hayo yaliyofanyika tarehe 10 – 11 Juni, 2025 yalifunguliwa rasmi na wataalamu mahiri wa taaluma, Prof. John Philemon na Prof. Dev Jani.**

**Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo washiriki katika maandalizi ya tafiti bora kwa kufuata misingi ya kitaaluma. Mada zilizojadiliwa kwenye mafunzo hayo ni pamoja na utangulizi wa tafiti za kitaaluma na umuhimu wa kuchapisha, mbinu za kufanya utafiti, kusoma na kuandika kwa ufanisi, uandishi wa utangulizi wa tafiti kwa kutumia mifano halisi ya vitabu na tafiti mbalimbali, pamoja na kufanya mapitio ya maandiko (Literature Review) kwa kufuata viwango vya kitaaluma.**



Wakufunzi wa ISW wakipata mafunzo kuhusu Uandishi wa Kitaalamu (Capacity Building on Academic Writing) yaliyofanyika Chuo cha Ustawi wa Jamii, Dar es salaam.




Mhadhiri Msaidizi Mary Mchau (mwenye koti jeusi katikati) akielezea huduma zinazotolewa na Chuo kwa mwananchi aliyetembelea banda la Chuo katika Maonesho ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Dodoma.

# HUDUMA ZA ISW ZAVUTIA WANANCHI MAONESHO YA UTUMISHI WA UMMA 2025

**Chuo cha Ustawi wa Jamii ni miongoni mwa vyuo vya elimu ya juu ambavyo vilitoa huduma kwa wananchi wa mkoa wa Dodoma katika maonesho ya Kitaifa ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2025 ambayo yalianza tarehe 16 - 23 Juni, 2025 katika Viwanja vya Chinangali Park – Dodoma.**

**Katika maonesho hayo, Chuo cha Ustawi wa Jamii kilitoa huduma mbalimbali kwa wananchi waliotembelea banda hilo. Huduma zilizotolewa wakati wa maonesho hayo ni, ushauri na msaada ya kisaokolojia, Ushauri wa kitaaluma na maelezo kuhusu huduma zinazotolewa na Chuo cha Ustawi wa Jamii katika kampasi kuu ya kijitonyama, Dar es salaam pamoja na kampasi ya Kisangara, Mwanga iliyopo mkoani Kilimanjaro. Huduma za udahili kwa program za kitaaluma kwa mwaka wa masomo 2025/2026 pia zilitolewa katika maonesho hayo.**

**Maonesho hayo yameimarisha uhusiano kati ya Chuo na jamii na kuwezesha jamii kupata ufahamu mzuri kuhusu mchango wa Chuo cha Ustawi wa Jamii katika kukuza maendeleo endelevu katika jamii.**




Afisa Udahili Bernadeta Kimario (wa kwanza kushoto) akisalimiana na kugawa kipeperushi cha Chuo kwa mwananchi aliyetembelea banda la Chuo katika Maonesho ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Dodoma.



isw_official_tz   isw_official_tz   taasisiyaustawi   isw_official_73   www.isw.ac.tz



Wanafunzi wakipokea maelezo kutoka kwa Maafisa Wakutubi kuhusu huduma za maktaba ya Chuo katika Maonesho ya Wiki ya Maktaba yaliyofanyika ISW, Dar es salaam.

# MAONESHO YA WIKI YA MAKTABA YAWAJENGEA WANAFUNZI UELEWA MPYA

**Idara ya Maktaba ya Chuo cha Ustawi wa Jamii iliandaa Maonesho ya Wiki ya Maktaba yaliyofanyika kuanzia tarehe 16 - 20 Juni 2025 katika viwanja vya Chuo cha Ustawi wa Jamii. Maonesho hayo yalilenga kuwapatia wanafunzi, watumishi na wadau mbalimbali fursa ya kipekee ya kujifunza, kuelimika na kufahamu kwa kina huduma mbalimbali zinazotolewa na Maktaba ya Chuo.**

**Wanafunzi walipata nafasi ya kutembelea banda la maonesho na kushiriki kikamilifu kwenye mawasilisho na mafunzo yaliyotolewa na Maafisa Wakutubi. Huduma zilizotolewa katika banda hilo ni pamoja na maonesho ya vitabu vipya vinavyopatikana katika maktaba, huduma za maktaba za kielektroniki kama vile BUKU, Research for Life na Cotul, ambazo husaidia wanafunzi na wakufunzi kupata rasilimali za kitaaluma kwa njia ya mtandao.**

**Aidha, maelezo ya jinsi ya kutumia mifumo ya kufanya marejeo (referencing skills) yalitolewa kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi kuandika kazi za kitaaluma kwa kufuata viwango vinavyokubalika kitaaluma. Washiriki pia walipata uelewa wa kutumia mfumo wa KOHA, unaotumika na Chuo kusimamia huduma za maktaba, pamoja na kuelekezwa utaratibu sahihi wa kuazima na kurejesha vitabu.**



Watumishi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii wakisikiliza kwa umakini mada zilizokuwa zinawasilishwa katika Semina ya Afya ya Akili, Uraibu na Homa ya Ini iliyofanyika Chuo cha Ustawi wa Jamii, Dar es salaam 21 Juni, 2025.

# WATUMISHI WA USTAWI WAPATIWA SEMINA YA AFYA YA AKILI, URAIBU NA HOMA YA INI

**Chuo cha Ustawi wa Jamii kiliendesha semina kuhusu Afya ya Akili, Uraibu na Homa ya Ini kwa watumishi wake tarehe 21 Juni, 2025. Semina hiyo ilifunguliwa na Mwakilishi wa Mkuu wa Chuo, Dkt. Happy Mwakajila, Mada mbali mbali ziliwasilishwa na Dkt. Rugemalila kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dkt. Patric Celestine kutoka Hospitali ya Mwananyamala pamoja na Rufina Khumbe – Mhadhiri Msaidizi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii.**

**Semina hiyo ilihudhuriwa na watumishi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii kampasi ya Dar es salaam. Semina ililenga kuwapatia watumishi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii maarifa na mbinu za kukabiliana na changamoto za kisaikolojia zinazoweza kuathiri utendaji kazi na ustawi wao kwa ujumla na kujikinga dhidi ya maambukizi ya homa ya ini.**



Mhadhiri Msaidizi, Rufina Khumbe akiwasilisha mada kuhusu mbinu za kukabiliana na changamoto za kisaikolojia.



Dkt. Rugemalila Mtaalam wa masuala ya afya ya akili kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa akiwasilisha mada kuhusu afya ya akili.



Mkuu wa Chuo Dkt. Joyce Nyoni akiongoza Mkutano wa tathmini ya mipango na utendaji wa Chuo cha Ustawi wa Jamii uliofanyika ISW, Dar es salaam 26 Juni, 2025.

# DKT. JOYCE NYONI AONGOZA MKUTANO WA TATHMINI YA MIPANGO NA UTENDAJI WA CHUO CHA USTAWI

**Mkuu wa Chuo cha Ustawi wa Jamii, Dkt. Joyce Nyoni, aliongoza mkutano muhimu tarehe 26 Juni, 2025 wenye lengo la kujadili na kutathmini utekelezaji wa mipango ya Chuo kwa mwaka wa fedha 2024/25. Mkutano huo ulifanyika katika ukumbi wa mikutano wa Chuo na ulihudhuriwa na watumishi kutoka idara na vitengo mbalimbali.**

**Katika mkutano huo, Dkt. Nyoni alisisitiza umuhimu wa kila mtumishi kutekeleza majukumu yake kwa weledi, ubunifu na uadilifu ili kufanikisha malengo ya Taasisi katika kutoa huduma bora kwa wateja wa Chuo, hususan wanafunzi na jamii.**

**Alieleza kuwa tathmini ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ni muhimu katika kujua mafanikio yaliyopatikana, changamoto zilizojitokeza na kuweka mikakati ya maboresho kwa kipindi kijacho. Aidha, Dkt. Nyoni alitumia fursa hiyo kusikiliza maoni, mapendekezo na changamoto kutoka kwa watumishi, akisisitiza kuwa ushirikishwaji wa watumishi katika maamuzi ni msingi wa ufanisi na uwajibikaji katika Taasisi.**



Watumishi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii wakisikiliza kwa makini hoja mbalimbali zilizokuwa zinawasilishwa katika mkutano huo uliofanyika ISW, Dar es salaam 26 Juni, 2025.



Mwakilishi wa Mkuu wa Chuo Dkt. Dominic Nkolimwa (aliyesimama) akizungumza na Wajumbe wa Kamati ya Dawati la Jinsia katika mafunzo maalumu kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia na ushauri nasihi yaliyofanyika ISW, Dar es salaam.

# WAJUMBE WAJENGEWA UELEWA KUHUSU MASUALA YA UKATILI WA JINSIA NA USHAURI NASIHI

**Chuo cha Ustawi wa Jamii, kupitia Dawati la Jinsia, kiliendesha mafunzo maalum kwa wajumbe wa Kamati ya Dawati la Jinsia kwa lengo la kuwajengea uelewa mpana kuhusu masuala ya Ukatili wa Kijinsia (Gender-Based Violence - GBV) pamoja na huduma ya ushauri nasihi kwa manusura wa ukatili huo. Mafunzo hayo yalifanyika katika kampasi ya Dar es Salaam tarehe 28- 29 Juni, 2025.**

**Mafunzo hayo ni sehemu ya jitihada za Chuo katika kuimarisha mifumo ya ulinzi na usaidizi kwa wahanga wa ukatili, sambamba na kuandaa watendaji waliobobea katika kushughulikia kesi hizo kwa weledi.**

**Mafunzo hayo yalijikita katika maeneo muhimu ikiwemo aina na dalili za ukatili wa kijinsia, ambapo washiriki walielimishwa kuhusu namna ya kutambua vitendo vya ukatili wa kimwili, kijinsia, kisaikolojia na kiuchumi, ambavyo mara nyingi hujificha katika mila, desturi na mfumo dume unaotawala katika baadhi ya jamii.**



Wajumbe wa Kamati ya Dawati la Jinsia wakiwa wanapata mafunzo ya masuala ya ukatili wa kijinsia na ushauri nasihi yaliyofanyika ISW, Dar es salaam.



Wahitimu wa Uanagenzi na Wanafunzi wakiwa wanasikiliza hotuba ya mgeni rasmi Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma Prof. Sotco Komba katika hafla ya utoaji vyeti kwa Wahitimu wa Uanagenzi iliyofanyika ISW, Dar es salaam 28 Juni, 2025.

# HAFLA YA UTOAJI VYETI KWA WAHITIMU WA UANAGENZI

**Naibu Mkuu wa Chuo (Taaluma), Prof. Sotco Komba, aliwatunuku vyeti wahitimu wa programu ya uanagenzi wanafunzi waliokamilisha mafunzo kwa vitendo katika taasisi mbalimbali tarehe 28 Juni, 2025.**

**Prof. Komba aliwahimiza vijana kutumia fursa zilizopo chuoni na kutoa wito kwa taasisi mbalimbali kuendelea kutoa nafasi za mafunzo kwa vitendo ili kuwajengea wahitimu uwezo wa kujiajiri.**

**Wamiliki wa taasisi ambao walihudhuria katika hafla hiyo walikipongeza Chuo kwa kuanzisha programu yenye mchango mkubwa kwa maendeleo ya vijana, wakisisitiza umuhimu wa kuendelezwa.**

**Aidha Wahitimu walitoa ushuhuda wa namna mafunzo hayo yalivyowawezesha kiujuzi na kitaaluma.**



Naibu Mkuu wa Chuo (Taaluma) Prof. Sotco Komba akitoa hotuba kwa Wahitimu wa Uanagenzi na Wageni waalikwa.




Mhitimu akipokea cheti cha pongezi kutoka kwa Naibu Mkuu wa Chuo (Taaluma) Prof. Sotco Komba baada ya kuhitimu mafunzo ya Uanagenzi.

# KURASA RASMI ZA CHUO CHA USTAWI WA JAMII

**INSTAGRAM**
ISW_OFFICIAL_TZ

**TWITTER (X)**
TAASISIYAUSTAWI

**WHATSAPP CHANNEL**
CHUO CHA USTAWI WA JAMII

**YOUTUBE CHANNEL**
ISW_OFFICIAL_73

# CHUO CHA USTAWI WA JAMII

210 Shekilango Road

P.O. BOX 3375

14113 Kijitonyama

Dar es Salaam

+255735509090

+255677111200

+255716121096

or

info@isw.ac.tz